**Nambari ya Mtahiniwa ____________________**

**SMZ**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA**

**133 KISWAHILI**

**MUDA: SAA 2.00 JUMATATU 01 NOVEMBA, 2021 MCHANA**

## MAELEKEZO KWA WATAHINIWA

1. **Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.**
2. **Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MANNE (4) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.**
3. **Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
4. **Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.**
5. **Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.**
6. **Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| 11. | | |
| 12. | | |
| JUMLA | | |

**Mtihani huu una kurasa 12 zenye maandishi**

**Nambari ya Mtahiniwa** ___________________

**SEHEMU A: (Alama 15)**

**UFAHAMU**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

1. **Soma habari hii kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.**

Latifa alikuwa ni mwana wa pekee. Wazazi wake walikuwa **wakwasi**. Hivyo Latifa alilelewa kama tunu na tamasha. Alidekezwa ajabu. Hakuna chochote alichokosa katika maisha yake.

Latifa alikuwa na dosari moja ya utovu wa nidhamu. Wazazi wake walizoea kumuita "Mami" kila walipokuwa wakimkosoa. Wazazi wake walijitahidi kumfunza umuhimu wa nidhamu, lakini wapi!

Katika jumba lao la kifahari, Latifa alikuwa na chumba chake, kilichokuwa na kila kitu, **runinga**, kompyuta na simu ya mezani. Wazazi wake hawakujali kujuwa kanda za video alizokuwa anatazama. Ingawa kulikuwa na runinga nyengine ukumbini, Latifa hakutazama asilani. Sababu aliyoitoa ni kwamba vipindi vyake vilikuwa "vina boa". Kutokana na aina ya malezi aliyolelewa Latifa, majirani, jamaa na marafiki waliwalaumu wazazi wake kwa kusema mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Wazazi nao hawakujali, hivyo walidai kwamba, waliowalaumu walikuwa washamba wasiojua kuwalea watoto wao kisasa.

Alipofika umri wa miaka kumi (10), Latifa aliandaliwa **karamu** kubwa ya ukumbusho wa siku ya kuzaliwa kwake. Walioalikwa ni wakwasi wa wakwasi wenye nafasi. Palikuwa na keki yenye daraja kumi, kwenye daraja la kumi palikuwa na mishumaha kumi yenye rangi tofauti ili kudhihirisha umri wa Latifa.

Kabla ya sherehe kuanza, Latifa alisema kwamba, angependa rafiki yake wa kiume akae karibu naye kama bibi na bwana harusi wafanyavyo. Kwa mara ya kwanza wazazi wa Latifa walikataa kutimiza ombi la mtoto wao kipenzi. Naye Latifa kwa hasira, alichukuwa zile keki na kuwatupia wageni usoni, akianzia na wazazi wake. Wazazi wake walishikwa na bumbuazi na **tahayuri**, nyuso zao hawakujua pakuziweka. Wageni hawakuamini macho yao. Wasichana wenzake walimfuata Latifa chumbani alikojifungia.

Watoto wa mtaani na majirani waliokuwa wamefungiwa nje ya mlango mkuu, walijialika katika karamu. Walipata bahati wasiyoilalia wala kuiamkia. Walifurahia uhondo ambao hawajawahi kuuonja maishani mwao. Waliimba nyimbo za sifa na kumtakia Latifa maisha marefu.

**Maswali**

a) Eleza funzo kuu la hadithi hii.

___

___

___

b) Latifa alikuwa na kasoro gani?

___

___

___

c) Kwa nini majirani waliwalaumu wazazi wa Latifa?

___

___

___

d) Bainisha sababu iliyowafanya wazazi wa Latifa kushikwa na bumbuazi?

___

___

___

e) Lete maana ya maneno yafuatayo.

i. Wakwasi

___

___

ii. Runinga

___

___

iii. Karamu

___

___

iv. Tahayuri

___

___

2. Fupisha aya ya tatu (3) ya habari uliyoisoma hapo juu kwa maneno yasiyozidi ishirini na tano (25).

## SEHEMU B: (Alama 40)

## SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

**Jibu maswali MANNE (4) katika sehemu hii. Swali la sita (6) ni la lazima.**

3. a) Andika mfano wa sentensi zenye miundo ifuatayo.

   i. W+T+N

   ii. N+T+E+E

   iii. I+N+V+t+V

   b) Kwa kutumia mifano eleza maana ya istilahi zifuatazo.

   i. Sentensi ambatano

ii. Viunganishi

____________________

____________________

____________________

____________________

4. a) Tunga sentensi kwa kutimia vihusishi vifuatavyo.

Nambari moja (i) imetumika kama mfano.

i. Baada ya

Mgonjwa aliruhusiwa baada ya kupata matibabu.

ii. Kwa

____________________

____________________

iii. Mbele ya

____________________

____________________

iv. Kando ya

____________________

____________________

b) Andika sentensi zifuatazo katika hali ya wingi.

i. Dawa inayolevya ni hatari.

____________________

ii. Kiti kimekatika katikati.

____________________

5. a) Bainisha hatua tatu (3) za mwanzo za ufupisho wa habari.

i. ____________________

____________________

ii. ____________________

____________________

iii. ____________________

____________________

b) Tafsiri sentensi zifuatazo kwa lugha ya Kiswahili.

i. Our students have scored high marks in Mathematics.

_____________________________________________

ii. Twenty times fifteen is equal to three hundred.

_____________________________________________

6. a) Tafsiri sentensi zifuatazo kwa lugha ya Kiingereza.

i. Wageni watasafiri asubuhi mapema.

_____________________________________________

_____________________________________________

ii. Zawadi anazungumza Kiswahili kwa ufasaha.

_____________________________________________

_____________________________________________

iii. Mwalimu wangu anasomesha vizuri.

_____________________________________________

_____________________________________________

b) Andika nambari zilizokosekana katika tarakimu zifuatazo.

Swali nambari moja (i) limetumika kama mfano.

i. 2,500,000, <u>3,000,000</u>, <u>3,500,000,</u> 4,000,000

ii. 1,000,100, ___________, _____________, _____________, 1,000,500

iii. 5,000,007, 5,000,008, _____________, ____________, ____________

7. a) Andika sentensi zifuatazo kwa kuzingatia vituo na taratibu za uandishi.

i. tanzania ni moja kati ya nchi za afrika mashariki

_____________________________________________

_____________________________________________

ii. baba humwagilia mimea asubuhi mchana na usiku

_____________________________________________

_____________________________________________

iii. Loo ameumia vibaya sana

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

b) Toa mifano miwili (2) ya mada zinazoweza kufanyiwa mdahalo.

i. ______________________________________________________________________

ii. ______________________________________________________________________

**SEHEMU C: (Alama 30)**

**FASIHI**

**Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii.**

8. a) Tunga beti tatu (3) za utenzi unaohusu virusi vya Corona.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

b) Andika ujumbe unaopatikana katika utenzi ulioutunga hapo juu.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

9. Oanisha methali kutoka **ORODHA A** na zile zinazofanana kutoka **ORODHA B** kwa kuandika herufi ya jawabu katika mabano.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i. Kambare mkunje angali mbichi. ( ) | a) Polepole ndio mwendo. |
| ii. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu. ( ) | b) Kidole kimoja hakivunji chawa. |
| iii. Haraka haraka haina baraka. ( ) | c) Bendera hufuata upepo. |
| iv. Damu nzito kuliko maji. ( ) | d) Udongo upate ulimaji. |
| v. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. ( ) | e) Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. |
| | f) Adui wa mtu ni mtu. |
| | g) Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe. |
| | h) Bora kinga kuliko tiba. |

10. Kwa maneno yasiyopungua 120 na yasiyozidi 130 andika hadithi inayotufundisha ubaya wa usaliti.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

Nambari ya Mtahiniwa ____________________

**SEHEMU D: (Alama 15)**

**UTUNGAJI**

**Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.**

11. Andika Insha ya maneno kati ya 120-130 yenye kichwa cha habari "AJIRA ZA UTOTONI"

12. Eleza mambo matano (5) yanayopaswa kuzingatiwa katika uandishi wa matangazo ya biashara.

**Nambari ya Mtahiniwa ____________________**

.................................................